



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO

**Unapojibu tafadhali taja:**

Kumb. Na. HWB/L.20/5/VOL.XXI.73

Tarehe: 27 Julai, 2022

Mkurugenzi Mtendaji,  
Africa Steel Company Limited,  
S.L.P 8513,  
**DAR ES SALAAM**

Yah: **UTHIBITISHO WA MATUMIZI NA UMILIKI WA ARDHI**

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu, rejea barua yako ya tarehe 21 Julai, 2022 inayotutaka kuwapa uthibitisho wa eneo lenu mlilopewa na Kijiji cha Mwavi kwaajili ya Ujenzi wa kiwanda cha Nondo.

2. Baada yakupata barua yenu tumefanya ukaguzi wa eneo lenu uwandani (saiti) na kufanya majadiliano na Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji cha Mwavi pamoja na Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwavi, wote kwa pamoja wamekiri kuwa wametoa eneo hilo la Kijiji kwa mwekezaji AFRICA STEEL COMPANY LIMITED kwa kufuata utaratibu wote wa mikutano ya kisheria ya kijiji cha Mwavi.

3. Pamoja na barua yenu kunamaswali ambayo mlitaka kupatiwa majibu kutoka Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji

- Hoja ya kwanza mliomba kufahamishwa kama eneo mlilopatiwa limeweza kutumika kwa matumizi ya kiwanda. Napenda niwafahamishwe kuwa eneo mlilopewa na Kijiji halina shida kwaajili ya Ujenzi wa kiwanda ingawa eneo lenu bado halina mchoro wa Mpango Miji unaoonesha matumizi ya kiwanda, hivyo Halmashauri ipo tayari kuwaandalia mchoro wa Mipango Miji wa matumizi ya kiwanda na kuwafanyia upimaji ili mwendelee kumilikishwa kama eneo la kiwanda
- Hoja ya pili ilitaka kufahamu kama kuna pingamizi lolote kuhusu umiliki wa eneo mlilopewa. Halmashauri ya wilaya ya Bagamoyo haina pingamizi lolote kuhusu eneo mlilopewa kwasababu eneo hilo lilikuwa chini ya Kijiji cha Mwavi. Halmashauri ya Kijiji imethibitisha mihtasari ya vikao vyake vya kisheria ikieleza kuwa eneo hilo lilikuwa mali ya Kijiji ambapo walilidhia kukabidhi kampuni yenu. Hivyo unashauliwa kukamilisha upimaji wa eneo lako mapema ili uwezo kumilikishwa na kuendelea na uzalishaji wa Nondo.

4. Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo inakaribisha sana wawekezaji hivyo inapenda kukutakia uwekezaji mwema ambao utaleta tija kwa nchi yetu.

Barua zote ziadikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, Barabara ya Uhindini, S.L.P. 59, 61301-BAGAMOYO.  
Mkoa wa Pwani.Simu Na: 023 2440164, Nukushi: 023 2440338 Barua Pepe: [ded.bagamoyo@pwani.go.tz](mailto:ded.bagamoyo@pwani.go.tz). Tovuti:

[www.bagamoydc.go.tz](http://www.bagamoydc.go.tz)

Wako katika Ujenzi wa Taifa



Majid S. Mhina  
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
BAGAMOYO.

MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA  
BAGAMOYO

